BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 21 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Afya:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Afya kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Afya ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

151. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Suala la udhalilishaji wa wanawake na watoto limekuwa likiongezeka siku hadi siku na kupelekea kesi nyingi kukosa kutolewa hukumu kwa wakati na kusingizia kuwa mashahidi wa kesi hizo hawafiki mahkamani.

(a) Je, Serikali imechukuwa hatua gani kwa wale mashahidi ambao hukataa kwenda mahkamani kutoa ushahidi.

(b) Je, wapo mashahidi waliowahi kutumiwa Hati ya Kukamatwa (Arrest Warrant) baada ya kukataa wito wa mahkama wa kufika na kutoa ushahidi.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

49. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia jemedari wetu na muasisi wa Mapinduzi ya mwaka 1964, Marehemu Mzee Abeid Aman Karume alitangaza wazi kwamba Zanzibar haina wafungwa wala haina jela, isipokuwa ina Vyuo vya Mafunzo na wale waliofanya makosa na kuwekwa katika vyuo hivyo ni wanafunzi na wamewekwa humo kwa ajili ya kurekebishwa tabia pamoja na kupata mafunzo yatakayowawezesha kujitegemea watakapomaliza muda wa kutekeleza hukumu zao.

Je, ni mafunzo gani wanapewa wanafunzi hao (wafungwa) zaidi ya kilimo cha jembe la mkono pamoja na kufanyishwa kazi za nguvu katika mafunzo yote yaliyopo Pemba na Unguja.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

97. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa mujibu wa takwimu za kibajeti, pesa nyingi za miradi ya maendeleo ya Serikali zina mahusiano ya moja kwa moja na kazi za uhandisi. Hata hivyo, kumekuwa na mapungufu makubwa yaliyokithiri katika utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ya Serikali kwa sababu kubwa ya kukosa usimamizi kutoka hatua za mwanzo hadi mwisho.

Je, kwa nini Serikali haioni haja ya kuwa na Afisi ya Muhandisi Mkuu Huru wa Serikali kama ilivyo katika nchi nyingi zinazoendelea na zilizoendelea.

<u>**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**</u>

102. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo jema kwamba, Serikali imeamua kujenga barabara mpya nyingi za mijini na vijijini ili kurahisisha shughuli za kijamii nchini. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa mpango huu hauonekani kwenda sambamba na Mpango Mkuu wa Usafirishaji Zanzibar wa mwaka 2009 (Zanzibar Transportation Master Plan (ZTMP 2009).

Je, ni kilomita ngapi za barabara zilizokusudiwa ziko ndani ya ZTMP 2009 na ngapi zinahitaji mapitio ya ZTMP 2009.

<u>**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**</u>

119. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa miaka mingi Zanzibar imekuwa ya mwanzo kuliko maeneo mengi ya Afrika Mashariki katika sanaa ya maigizo kupitia TVZ sasa ZBC. Katika wakati huo michezo mbali mbali ya sanaa ya maigizo ilitamba sana kwa kuburudisha na kuelimisha, hali iliyopelekea kupendwa sana na wananchi wengi, ikiwa ni pamoja na michezo ya Dokta Ayubu, burudani za Mashaka na Binjiwa, Halikuniki na Sekembuke, Makombora na wengineo.

(a) Je, Wizara yako imefanya utafiti upi ili kujua kwanini sanaa za maigizo zimefifia Zanzibar.

(b) Je, Wizara imefanya mpango gani wa kuhuisha sanaa hiyo.

(c) Je, Wizara yako imefanya utafiti wowote wa kuwatambua wadau na wasanii wa maigizo, kukaa nao na kujua changamoto zinazoikabili sanaa hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

129. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inapofanya zoezi la uchimbaji wa visima hutumia gharama tofauti kwa kila kisima.

Je, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kupanga viwango vya gharama ya uchimbaji wa visima Zanzibar.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

141. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu. Na kwa kuwa katika maeneo ya Bungi hasa yale maeneo yanayolimwa zao la vanila, hivi sasa pana uharibifu wa mazingira hasa ukataji wa miembe na jamii ya michungwa, kiasi ambacho hakivumiliki na mtu yeyote.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inayo habari ya kukatwa miti hiyo.

(b) Je, Mhe. Waziri umechukua hatua gani juu ya mwekezaji yule wa zao la vanila katika eneo hilo.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

152. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Pamoja na udogo wa eneo la ardhi ya Zanzibar, imeonekana kuwa baadhi ya wananchi wanamiliki maeneo kwa muda mrefu bila ya kuyaendeleza na kusababisha usumbufu kwa wahitaji wengine.

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kutatua kadhia hii.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

78. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Zanzibar ni sehemu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo kupitia Muungano huo, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na pande zote mbili za

Muungano (Zanzibar na Tanzania bara). Kwa kuwa nchi mbili hizi ziliungana zikiwa na mamlaka sawa na tofauti ya idadi ya watu tu.

(a) Je, utatuzi umefikia wapi wa changamoto ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutakiwa kulipia kodi mara mbili kwa bidhaa zinazotokea Zanzibar kwenda Tanzania bara.

(b) Je, utatuzi wa suala la Zanzibar kuuza sukari yake Tanzania bara umefikia wapi.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

155. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaishukuru Serikali kwa kuifanyia matengenezo skuli yetu ya Uzini. Hata hivyo, gharama halisi ya matengenezo hayo haijawekwa wazi na kufahamika na wananchi wetu.

Je, Serikali imegharamia kiasi gani cha fedha kwa matengenezo ya skuli ya Umoja Uzini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Afya:**

Ripoti ya Wizara ya Afya kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**21 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**